

Kule kuja kwa Bwana

Mt. Matayo 24:32-51 kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja.

Biblia ilisema ya kwamba, “Kila kitu kitakuwa kikubwa sana katika siku ile kuhusu Yohana Mbatizaji hata mpaka milima yote itashushwa na mabonde yote yatajazwa.” Naam, Bwana. “Na mahali pote palipoparua patalainishwa.” (Isaya 40:3-5)

Mbona, ninaweza kuwazia nikiwaona kule, nafikiri Yohana angetokea, ama huyu mtangulizi wa heshima wa Kristo, na kuchukua jangwa lote na kulilainisha, na kulipanda nyasi tena, Mnaona? Loo! Wao, nawazia walikuwa wamepeana mambo yote, karibu kama vile walivyofanya leo. Mt Yohana 1:15-23

Lakini, lilikuwa ni jambo nyenyekevu sana, hata mitume walilikosa. Wao walisema, “Vema, mbona Maandiko yanasema, kama ninii.....unaenda kule ukatolewe sadaka sasa? Kwa nini Maandiko yanasema ya kwamba – ya kwamba eliya hana budi kuja kwanza?

Yeye akasema, “Yeye amekuja tayari, wala hamkumjua. Na, mwana wa Adamu, watamanyia jambo lile lile. Lakini, Yohana, “Yeye akasema, “alifanya yale hasa aliyoandikiwa kutenda. Nao walimtendea sawasawa tu na yale waliyopaswa kumtendea. Na, “Kasema, “vivyo hivyo Mwana wa Adamu atateswa.”

Mbona, hakukuwako, nafikiri, theluthi moja ya jamii yote ya Wayahudi waliopata kujua ya kwamba Yesu Kristo alikuwapo duniani. Hawakuninii.....Huenda walikuwa wamemsikia mshupavu Fulani wa dini kule chini mahali Fulani, lakini wao hawakumjali, waliendelea tu. “Alikuwa kwake, na walio wake hawakumjali, waliendelea tu. “alikuwa kwake, na walio wake hawakumpokea. “Yohana 1:11 sasa, ndipo ninapoamini hata....sasa, halikusema ya

kwamba angekuja kisiri. Lakini Unyakuo utakuwa ni siri. Kwa hiyo kama ilikuwa ni siri hivyo, yeye alipokuja, ni zaidi sana jinsi gani unyakuo hautajulikana! Mnaona? Wao hawatajua jambo hilo. Moja kwa moja watasema, “Vema, nilifikiri tulipaswa kuwa na unyakuo. Na ni vipi basi mikasa hii yote juu ya nchi” “

Yeye atasema, “Umepita tayari, nanyi hamkujua.” Unaona? Itakuwa hivyo, kama tu mwizi usiku. I Wath 5:1-11, 2Petro 3:10, Ufunuo 3:3:16:15)

Sasa, hivyo ndivyo itakavyo – itakanyotukia, na utakuwa umepita. Si kwamba, watahusha kundi Malaika, wakiwa na sepetu, na kuchimbua makaburi. Biblia ilisema. “Tutabadilishwa, kabla hata hajafumba na kufumbua jicho lako.” Kufumba na kufumbua (1kor 15:51-52) kila kitu kitakuwa kimekwisha, upesi namna hiyo.

Kusema tu, “Mtu Fulani ametoweka.”

Vema, nasikia kama tungeweza kuchunguza ulimwengu mzima, leo, kumekuwa na watu mia tano wanaotoweka duniani kila siku, unaona, hawajui kitu juu yake. Wao wanatokea tu, wanatoweka.

Vema, hakutakuwako na wengi sana watakaonyakuliwa.

Sasa, sitaki kuwashtusha, nami – nami si – si – sidhani ndiyo hivyo, lakini nataka tu kuwaambia yale yeye aliyosema. Nanyi mnajua hilo, ninyi wenyewe. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji. Watu wanane kutoka ulimwenguni, kuokolewa kwa maji” (I Petro 3:18-21)

Vema, unasema, “loo jamani! Hakuna haja ya mimi kujaribu. “Hiyo inaonyesha huna aina ya imani unayohitaji.

Kama kutakuwako tu – kutakuwako na mmoja, huyo atakuwa ni mimi, Amina, maana ninaamini. Unaona? Hivyo ndivyo unavyotakiwa uamini, unaona, “Atakuwa ni mimi.”hakika. Ninataka kuishi kujaribu sana na yeye, hivi kwamba nijue yeye atanichukua wakati atakapokuja. Ninaamini. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kama kuna....kama watu wengine wasiponyakuliwa nitakuwapo kwa neema yake. Maana yeye aliniahidi mimi hilo, nami nanajua ya kwamba nita

– nitanyakuliwa, maana yeye hawezi kusema uongo. Nami ninajua nafsi yangu na maisha yangu anashuhudia, nami ninajaribu kuishi kila siku kama tu kwamba yeye alikuwa anakuja, kwa hiyo nita – mimi nitakuwa ndiye huyo. Hivyo ndivyo jinsi unavyotaka kujisikia. “kama kutakuwako na wanane, mimi nitakuwa mmoja wa hao wanane; kukiwa na mia tano, mimi nitakuwa mmoja wa hao mia tano. Sijui habari za jamaa huyo mwingine, lakini mimi ninataka kuwa mmoja wa hao mia tano. “Unaona? Hivyo unapaswa kushikilia moyoni. Unaona?”

Na kama hushikili hilo moyoni namna hiyo, imani yako ina kasoro. Unaona? Bado huna hakika kwamba umeokolewa, basi. Unakisia tu jambo hilo. Usifanye hivyo. Vema.

Ni wangapi wanajua kuwa kuna tofauti kati ya kuonekana kwa Kristo (appearing) na kuja kwa Kristo? Bi maneno mawili tofauti. Sasa hivi ni kule kuonekana, na kuja kwake kutakuwa hivi karibuni. Anaonekana miongoni/katikati yetu, alifanya kazi alizowahi kuzifanya katika kanisa lake. Sasa, wewe ni sehemu ya hilo kanisa, na kwa Neema unaamini mimi ni mmoja wa, wa hilo kanisa.

Sasa, mimi siyo mhubiri Mnajua kwamba siyo sina Elimu ya kufanya hivyo. Wakati mwingine najisikia tutopenda kusimama hapa miongoni mwa watu wa Mungu, ambao wameitwa kwa ajili ya huduma hiyo. Kuna mitume, Manabii, Waalimu, Wachungaji, na wainjilist siyo wote ni mitume, siyo wote ni manabii, siyo wote ni waalimu, siyo wote ni wainjilist. Nimesimama hapa.....

Lakini huduma yangu ni tofauti na Mchungaji au Mwalimu mimi siyo na kama nilisema mambo nimekosa Nisamehe simaanishi hivyo. Lakini hii huduma yangu kumtangaza yeye, kwamba yupo hapa [2]

Utume wangu, ambao ninaamini Mungu ameniitia mimi.....Inabidi niseme vitu vya kibinafsi leo, kwa sababu nimewaambia nitafanya hivyo, na kuiambia dunia. Utume wangu, ninaamini, hapa duniani ni nini? Ni kule kutangulia kuja kwa Neno kuja kwa Neno ambalo ni kristo. Na kristo Ndani yake anao utawala wa miaka Elfu na ana kila kitu pale kwa sababu yeye ni Neno. [3]

Nabii alisema: Nataka kusema hili sijawahi kulisema kabla, lakini kutokana na maandiko, kutokana na Alivyosema katika mwaka wa 1933 kule mtoni chini pale. Yale Aliyosema, kila kitu kimetokea kikamilifu hasa. Ninaweza nisifanye mimi, lakini ujumbe huu utamtambulisha Yesu kristo kwa dunia “Kwa maana kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza , kadhalika ujumbe huu utatangulia kule kuja kwa pili” Ujumbe utaendelea. [4]

Na mara hii tena; Sikilizeni, ndugu, Ninawasihi sana au ninawapisha mbele za Kristo kwamba mshikilie sehemu yenu na muwe na utulivu, lakini kama mngekuwa wa kiroho mngekuwa Unaona? Je hamjui jambo la kwanza kabisa alilolisema pale chini mtoni? Hamkumbuki Alilosema? “Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wakoNi ujumbe utakaotangulia kule kuja kwa pili kwa Kristo. Hivyo Malaika wa Bwana alivyosema

Sasa, sasa angalia sasa “Kama Yohana Mbatizaji.....” Sasa, kila mmoja wenu amelisikia hilo. Mmelisoma katika vitabu, na kulisikia kutoka kwa watu waliokuwa wamesimama pale wakilisikia hilo na kila kitu kingine, Wakati Malaika Mwenyewe alipozungumza huo ujumbe, kama kwanza kwa Kristo, unatumwa na ujumbe, ambao utatangulia kule kuja kwa pili kwa Kristo” Sasa Ujumbe” [5]

Kanisa linapitia wakati wa uchungu wa uzazi je huwezi kufanya uamuzi wako sasa tukiwa uweponi pake? Nimewaonyesha Neno hasa, kile alichosema Angefanya. Lakini ni nini? Mwana wa Adamu Neno la Mungu ni kali kuliko upanga uwao wote, kupambanua Roho, hata siri zilizoko moyoni “(Waebrania 4:12-13).

Kama vile tu lilivyokuwa wakati lilipofanyika mwili hapa duniani ndani ya Mwana wa Mungu, sasa linafunuliwa na Mwana wa Mungu kwani Amekuja kumwita Bibi Arusi atoke kwenye hizi taratibu.

“Tokeni kati yao Mkatengwe nao “Asema Bwana Msiguse kitu kilichokichafu, na Mungu atawakaribisha. (2 Kor 6:17-18) uko tayari kusalimisha maisha yako yote kwa Mungu? Kama uko tayari kusalimisha maisha yako yote kwa Mungu? Kama uko tayari, Simama

kwa miguu yako na useme, Nitafanya hivyo kwa msaada wa Mungu nalikubali sasa hivi kwa vyote vilivyo ndani yangu”

Halleluyah Mungu apewe sifa Unamuamini yeye? Inua tu mikono yako na uombe pamoja nami. Tubu makosa yako, uchungu wa kuzaa, ni wa kuzaa, ni vigumu kufa.

Lakini kufa sasa hivi (Yohana 12:24-25) kufa toka katika kutokuamini kwako. Toka katika hilo Hili ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, kama vile tu Yesu alipokuja hapa duniani; Ni Yesu Kristo tena akiwa kati yenu, akithibitishwa.

Ibrahimu alimpokea mtoto muda tu (mtoto wa Ahadi) baada ya hilo kutendeka [Wakati Yehova alipomtokea Ibrahim] (Mwanzo 18) Na Yesu anakuja tena. Huyu ni Roho wake yuko katibu sana na dunia, karibu sana na kuja kwamba yuko tayari hukupokea wewe. Sasa inua mikono yako na uombe pamoja na mimi.

Bwana Mungu, waache makuhani wote washikiliao madhabahuni waache watu walie. Hebu ile Nguzo ya moto na ile Nguzo ya Wingu ipite ndani ya watu leo na kuwapa kuwa makini/timamu, Bwana, kwa ufahamu wa kujua uwepo wa Mungu aliyehai na Mwenyenzi Mungu. Jalia hilo Bwana wapokee Naomba maombi hayo kwa kila mmoja wao katika Jina la Yesu Kristo wajaze kila mmoja na Roho Mtakatifu yule ambaye hana Roho Mtakatifu Bwana, naomba kampeni hizi za uamsho, mkutano huu, zifungue sasa kushuka kukuu kwa Roho Mtakatifu katika ukuu na nguvu. Tunaomba wagonjwa waponywe, vipofu waone, viwete watembee. Tunaomba udhihirisho wa Mungu aliye hai uletwe miongoni mwa watu, kama ilivyokuwa mchana wa leo, na hebu watu walipokee hilo katika jina la Yesu Kristo ninaomba hilo [6]

Sikiliza kwa karibu sasa, usikose hili sasa! Angalia kulikuwa na wajumbe wanne, wajumbe wanne wa mauti waliuua mti wa Bibi Arusi. Hiyo ni sawa? Ilikuwa ni nini? Tunutu, Nzige, Parare, Madumadu (Yoeli 1:1-4) hiyo ni sawa? Wajumbe wanne wa mashetani ya kiroma, kanuni, yaliua huo mti. Mmoja alichukua matunda; mmoja alichukuwa majani; mmoja alichukua magome yake; mmoja alichukuwa uhai. Hiyo ni sawa? Wajumbe wane wa kanuni

waliua huo mti, wote kasoro mizizi tu. Na kama wajumbe wanne wa mauti waliuua huo mti. Wajumbe wanne wa uzima wanaurudisha huo mti.

Je unalipata hilo? Amen. Kwa maana Mungu alisema, “nitarudisha” (Yoeli 1:25-27). Ataenda kurudishia kwa namna gani? Kwa wajumbe wanne wa uzima wanaurudishia huo. Wakwanza alikuwa nani? Martin Futher, kuhesabiwa haki kwa Imani wapili alikuwa nani? John Wesley kwa utakaso watatu alikuwa nani? Pentekoste na kule kurudishiwa kwa karama, Roho Mtakatifu, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wanne alikuwa nani? Lile Neno nini? Lile Neno.

Kulikuwa na manabii wakuu wanne. Mmoja wao Martin Futher, alianza kuangaza Nuru. Ilikuwa ni Nuru ndogo, nguvu kidogo tu ya kuhesabiwa haki kwa imani baadaye akaja Wesley, yenye nguvu. Kutakaswa. Baada ya Wesley ikaja yenye nguvu kuliko yeye, Pentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa nabii mwingine aliye mkuu. Unaona? Lakini katika siku za mwisho Malaki 4:5-6. Eliya atakuja na Neno lenyewe hasa.

Neno la Mungu linakuja kwa manabii katika wakati wa jioni Nuru itakuja kurudisha na kukirudisha tena (Zakaria 14:7) Nini? Kugeuza mioyo ya watoto nyuma kwenye imani ya mababa: Nuru ya nne.

Wauaji wanne waliuondoa, wajumbe wanne waliuharibu huo wajumbe wanne wa mauti waliondolea mbali kwa kanuni; Wajumbe wanne wa haki wanaurudisha tena.

Tabiri Mwana wa Adamu, Mifupa hii yaweza kuishi (Ezekiel 37:1-14) Toa unabii je mifupa hii yaweza kuwa hai? Angalia zile hatua nne za mifupa ya Ezekiel ili mikavu mifupa ikijitokeza? Lakini uhai ulikuja pale tu, siyo pale ngozi ilipokuja juu yake, lakini upepo ulipovuma juu yake. Pale ndipo ilipoendelea. Wale wajumbe wanne wa uzima walipouleta nitawarudisha tena. “Nitawarudishia, hivi wema Bwana Halleluyah utukufu sifa kwa Mungu.

Ile Nuru ya nne itakuja ambayo itafanya ishara zile zile. Tazama. Kuhesabiwa haki kwa Imani kulirudisha ile nyama laini ya mti. Kutakaswa kulileta tena lile ganda. Mafundisho ya utakatifu. Ni nini

kilichorudisha tena yale majani? Wapentekoste. Ulikuwa ni nini? Wapentecoste, majani, kupiga makofi, shangwe, kushangilia: Pentecoste ni Nini? Cha nne ilikuwa ni Neno lenyewe. Neno limefanyika mwili, matunda ya uthibitisho wa kufufuka, ishara kwamba Kristo mwishoni, baada ya kupandikiza utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Madhehebu yakafa, na Kristo kwa mara nyingine amejuweka katikati yeye mwenyewe kama jiwe la kifuniko la Piramidi.

Mstari wa kwanza, kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, halafu kule kuja kwa kifuniko ni nini? Lile kundi la Roho Mtakatifu likichongwa, kiasi kwamba inaweza kulingana na huduma ile ile Aliyokuwa nayo wakati alipoondoka; Kwamba Wakati anaporudi tena itanasa kitu chote katika unyakuo, ambapo wamehesabiwa haki kwa imani, wametakaswa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ile piramidi itasimama tena. Nyumba ya Mungu itaishi tena ule mti wa uzima unakua tena [7]

Kama mtu yoyote atawaambia kwamba wanajua ni lini Anakuja, unajua wamekosea kwa kuanzia, kwa sababu hakuna mmoja ajuaye hilo. Lakini tunataka tuishi leo kama kwamba ni sasa hivi.

Nataka kila siku nifanye kama vile ambavyo ningefanya wakati anakuja na sijui mahali pazuri zaidi ya kukutwa nikiwa kwenye huduma yangu, mahali pangu katika huduma kwa hiyo tunaendelea mbele mpaka atakapokuja [8]

Ninashukrani kwa kanisa la dunia nzima, linaloshinda, ambalo tayari limechaguliwa kimbele, na limeitwa na kutiwa Muhuri, na kukusudiwa katika ule mwili. Ninawaona hao kule Asia, Africa, Roma, na kila mahali, Indiana, na sehemu mbalimbali za U.S.A Africa. Kila mahali duniani kote ninaliona lile kanisa linaloshinda, ambaye unajua kwamba umekuja katika mwili. Katika Biblia yako ulisema, “Kila Roho ambayo haikiri hili, ni roho isiyo sahihi, ya mpinga Kristo. Kila Roho ambayo haishuhudii jambo hili hili, kwamba Kristo amekuja katika miili yetu, ni roho ya Mkristo” (1 Yohana 4:1-3; 2 Yohana 7) [9]

Sasa, nimekuwa nikizungumza nanyi kwa namna Fulani juu ya ujumbe, waziwazi sana. NamiWatu Fulani huenda wakawa na

wazo kwamba-kwamba mimi nadhani ya kwamba Yesu atakuja asubuhi ama usiku wa leo. Ndivyo ninavyodhani. Naam, sisemi ya kwamba yeye atakuja. Na, tena huenda yeye asiye hata juma lijalo, na huenda ikawa mwaka ujao, huenda ikawa miaka kumi. Sijui atakapokuja. Lakini kuna jambo moja nataka ku....daima mliweke mawazoni, mwa tayari kila dakika ama saa. Mnaona? Ili kwamba, kama hatakuja leo, huenda yeye akawa hapa kesho. Kwa hiyo liwekeni hilo mioyoni mwenu, ya kwamba yeye yuaja.

Na sijui ni wakati gani utakuwa muda wangu wa mwisho hapa duniani, wala hakuna mmoja wetu ajuaye. Na hakuna mmoja wetu ajuaye ni wakati gani yeye atakapokuja. Hata yeye hajui, yeye Mwenyewe, kwa maneno yake mwenyewe; yeye alisema, “Baba pekee, ndiye ajuaye yeye atakuja lini: hata mwana hajui yeye atakuja lini. “Ni wakati Mungu atakapomtuma kwetu tena. Bali tunakutazamia kuja kwake. Na iwapo hatakuja katika kizazi changu, huenda akaja katika kile kijacho; kama hatakuja katika hicho, atakuja katika kile kifuatacho. Lakini, kwangu mimi, ni vigumu kuona wakati wowote uliosalia. Mimi tu....Kwangu mimi, ingeweza kutukia dakika yoyote. Sasa, hilo halimaanishi...Hilo halimaanishi, sasa, ya kwamba utaona mbingu zikibadilika na kila....Huko siko kule kuja ninakozungumzia. Ninazungumzia kuhusu kunyakuliwa.

Mnaona, anatimiza kuja kutatua. Anakuja katika matatu ya wana, majina. Yeye alikuja katika utatu; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mnaona, yote hayo Kristo yeye yule, Mungu yeye yule daima. Naam tunajua alikuja kuleta kazi tatu za neema; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kila kitu, katika Mungu, kinakamilishwa katika tatu – tatu.

Na kwa hiyo alikuja mara ya kwanza, kumkomboa Bibi-Arusi wake. Anakuja mara ya pili, kama kunyakuliwa, kumchukua Bibi-Arusi wake. Anakuja, mara ya tatu, pamoja na Bibi-arusi wake, mfalme na Malkia; baadaye, hapo ndipo watu wengi wanakutarajia kule kuja.

Bali anapokuja wakati huu, katibu hakuna mtu yeyote ila wale walio tayari watajua wakati ajapo. Kutakuweko na kukosekana kwa watu. Hawatajua kilichowapata. Wao watanyakuliwa tu, katika dakika moja na kwamba watakosekana. “watabadilishwa katika dakika moja,

katika kufumba na kufumbua. “Kwa hiyo iweni tayari kwa ajili ya jambo hilo. Litakuwa jambo la kuchukiza hivi karibuni asubuhi kumkosa mpendwa hakukaa anayeweza kuwapata. Si ingekuwa vibaya sana kujua tayari kumepita nawe umekukusa? Kwa hiyo jiweke tu mbele za Mungu. [10]

Mara Nyingine tena: kule kuja kwa kwanza kwa Kristo anayepatikana na mauti. Anakuja mara tatu Kristo yuko katika hali tatu. Kuja kwa kwanza, alikuja kama anayepatikana na mauti ili amwage damu na kufa. Hiyo ni sawa? Huko ni kuja kwake kwa kwanza. Kule kuja kwa pili ni unyakuo. Tunakutana naye katika mawingu-asiyepatikana na mauti- akiwa ni Mungu katika umbo la kibinadamu. Amen! Mungu Emanuel atawale duniani. Hiyo ni sahihi. Mara tatu tu [11]

Hawa ni wale, Bwana, ambapo umetupa katika huduma mbali na wale wengine aliolala nchini kote, na duniani kote. Makaburini hapa yameshikilia wengi na hawa wanaongojea, watakatifu waliobarikiwa. Lakini ni kama vile ilivyosemwa/ilivyonenwa, sisi tulio hali tutakaosalia hatutawaziwa wale walikwisha kulala. Tarumbeta Italia waliokufa watafufuka kwanza: halafu tutanyakuliwa nao (1Wathesalonike 4:13-17)

Wakati utukufu wa Mungu utakapokuwa juu ya nchi, itaificha kanisa mbali na dunia. Haitawaona wakati wanaondoka.

Baba Mungu waweke hawa mkononi mwako. Ni wako ninawaomba, Mungu kwamba tutatembea siku zote kwa unyenyekevu mbele zako. Hatujui ni muda gani. Hatuhitaji kujua itachukuwa muda gani; siyo wajibu wetu, huo ni wajibu wako. Siyo mapenzi yetu kujua lini unakuja; ni mapenzi yetu beana utuweke wanyenyekeve mpaka utakapokuja. (1 Petro 5:5-7) na kutembea na wewe. Ni shauku yetu kuwa wewe uache ujulikane mara moja moja, Baba kati yetu, ili tuone kwamba bado tunatembea na wewe.

Tusamehe dhambi zetu zilizopita. Tuongoze sisi na utulinde kutokana na mitego ya shetani kwa siku za baadaye. Tuongoze sisi na utuelekeze sisi, oh Mungu Baba yetu. Sisi ni waliokataliwa na jumuiya za duniani, na madhehebu ya makanisa. Tunauona mwisho na tunashukuru wewe kwa macho ya kiroho katika Neno lako kuuona

wakati wa mwisho. Kwa maana mambo haya yote lazima yeye kwenye kule kupigwa mawe kukuu kutoka mbinguni (ufunuo 16:17-21). Rusaidie sisi; Bwana, tusije tukawa hapa katika siku hiyo lakini twende katika uwepo wako, tukirukia kifuni mwako. [12]

Sasa, Israeli waliobakia hawainui mapaka wakati wa ufufuo wa jumla. (ufunuo 20:11-15; Yohana 5:28-29). Na sasa wakati wa kuja kwake Bwana Yesu, wale ambao wanapenda kweli kule kuja kwake, ambapo wanaishi kwa jili ya hilo, wakati atakapo-onekana katika mawingu, kanisa la ambalo wamekufa katika kristo watainuka na wengine watabadilishwa katika muda mfupi wengineo wote wasijue chochote juu ya hilo kumbuka, aliwatokea wale waliokuwa mjini (Matayo 27:51-53), unaona unyakuo utakuwa kama hivyo. Tutaonana sisi kwa sisi halafu tutawaona wao. Dunia iliyobakia hawatawaona wao. Itakuwa kunyakuliwa kwa kisiri, tunangojea muda huo, halafu kurudi tena duniani kwa ajili ya ule utawala wa utukufu wa miaka elfu, halafu miaka elfu. Wafu waliobakia hawatakuwa hai kwa miaka elfu na halafu kuja kwa ufufuo wa jumla ambapo waisrael wote..... (ufunuo 20:4-6) [13]

Mpende Yesu kwa moyo wako wote kuwa tu mtu tahisi usijaribu kuwazia juu ya chochote; kuwa mtu rahisi mbele za Mungu kwa sababu kadiri unavyojaribu kuwazia ndivyo unavyokwenda mbali na yeye unaona? Kitu rahisi tu muamini yeye.

Sema “Sasa, vema atakuja lini? Kama anakuja leo, Vema kama anakuja miaka ishirini kutoka sasa, bado ni vizuri. Nitaendelea tu kama nilivyokuwa ninaendelea – kumfuata yeye bwana kama unaweza kunitumia mimi mahali popote, niko, hapa Bwana. Kama ni miaka mia kutoka leo, kama kijukuu wa kijukuu wa kijukuu wa mjukuu wangu bado nitaishi kumuona yeye akija, Bwana sijui itakuwa lini, lakini hebu tu nitembee sawa leo, pamoja na wewe, kwa sababu nitainuka katika siku ile sawa tu na nilivyolala kidogo mahali Fulani [14]

Ninaamini kwamba tunaishi wakati wa mwisho nafikiria karibu kila mtu ambaye.....wanaosoma au kuamini maandiko wanajua kwamba sasa tuko wakati wa mwisho wa historia ya dunia hakuna sababu ya kuiandika kwa sababu haitakuwepo tena mtu wa kuisoma. Ni wakati

wa mwisho. Ni basi? Sijui itachukuwa muda gani, hata malaika Mbinguni hawajui dakika au saa. Lakini tumeambiwa na Bwana Yesu kwamba tunayaona mambo haya yaanzapo kutulia tuinue vichwa vyetu kwa maana ukombozi wetu umekaribia (luka 21:25-28) [15]

Ninamshukuru Mungu kuwa ninaishi wakati huu wa kufungwa kwa matukia ya historia ya ulimwengu, sijui kama ningekuwa na cha kusema kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, na Mungu angeonyesha mpango wote kwangu mimi na akaniambie, “Ninataka wewe uwe mhubiri. Na sasa, ni wakati gani ungependelea kwenda duniani kuhubiri?”Ningechagua wakati huu, kwa sababu nafikiri huu ni wakati wa dhahabu.

Hakika ningependa niwe hapa wakati ule yeye alipotembelea duniani, lakini bado nafikiria hili sasa hivi, ni wakati mkuu kwa sababu ni wakati ambao anakuja kuchukua watu aliowakomboa, tulikaribia ufufuo wakati wote waliokombolewa watakapoinuka. Ni wakati wa utukufu wa namna gani kuzungumza na watu wanokufa wakati mkuu.

Lakini tunaliwa furaha/shauku juu ya hilo. Na tunajua kwamba historia inamalizika. Historia ya dunia karibu itaisha. Halafu tutaingia katika siku mpya, kwenye millennia ile kuu. Ambaye muamini mmoja wao, Ninaamini juu ya milleniam, millennium kutawala pamoja na Kristo, miaka elfu juu ya dunia; kule kurudi katika mwili kwa Bwana Yesu kuchukuwa watu walio mwilini, waliotukuzwa na Damu yake inayoosha inayotakasa [16]

Nukuu za Kiingereza

[1] “Ule muhuri wa tatu kitabu cha mihuri” uk 238-239

[2] “Kutoka wakati ule” (62-0713) Aya 102

[3] “Lile Neno lililonenwa ndiyo mbegu ya Asili” (62-0318M) Uk 20

[4] “Kumtazama Yesu” (63-1229E) uk 7

[5] “Maswali na majibu” (61-01112) kitabu cha CO uk. 571 Aya 384-385

[6] “Utungu wa uzazi” (65-0124) uk 40-41

[7] “Kurudishiwa Mti wa bibi Arusi” uk 75-76

[8] “Ule muhuri wa tatu kitabu cha mihuri” uk. 230-231

[9] “Ishara kuu” (59-1227M) aya 144

[10] “Mabirika yavujayo (964-0726) Aya 12-15

[11] “ Ule muhuri wa nne” kitabu cha mihuri uk. 308

[12] “Kujaribu kumtendea Mungu kazi” (65-0718M), Aya 193 – 195

[13] “Nitawezaje kushinda” aya 61

[14] “Ule muhuri wa sita” kitabu cha mihuri uk 450

[15] “Wapakwa mafuta wa siku za mwisho” Aya 17

[16] Muungano usioonekana uk. 6-7

Jiwe la kiroho la kujengea na. 159 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberge, Germany Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Charles E. Y. Kanju

Box 5138, Tanga

E-mail: chaelika@hotmail.com

cellphone: 0784 704299